

## **KIONGOZI CHA MWANAKIJIJI KATIKA USHIRIKISHWAJI WA MIPANGO NA USIMAMIZI WA MATUMIZI BORA YA ARDHI VIJIJINI**

Kijitabu hiki kimetolewa kama Kiongozi (kilichoboreshwa zaidi kulingana na wakati) cha Mwanakijiji katika Ushirikishwaji wa Mipango na Usimamizi wa Matumizi Bora ya Ardhi (Participatory Land Use Management – PLUM) na utekelezaji wa Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Na. 6 ya 2007 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya 1999. Kijitabu hiki kinafuatia toleo la kwanza (2000) na toleo la pili (2006) la Kiongozi cha Mwanakijiji katika Ushirikishwaji wa Mipango na Usimamizi wa Matumizi Bora ya Ardhi Vijini.

Kwa kutambua kuwa ardhi ni rasilmali ya msingi na jukwaa la maisha ya binadamu, ambayo tunaitumia kwa kuzalisha mazao, kufugia mifugo, kuhifadhia wanyamapori na misitu, kujenga nyumba, huduma n.k; hapana budi watumiaji wa ardhi tuweke utaratibu na mipango ya matumizi yake.

Mipango na Usimamizi wa Matumizi Bora ya Ardhi huweka utaratibu wa matumizi ya rasilimali za ardhi kwa kutatua migogoro, kuimarisha miliki za ardhi na matumizi yake, kugawa ardhi na kuboresha matumizi na hifadhi ya ardhi, kulingana na mapendekezo na uwezo wa walengwa. Huu ni mchango mahususi katika maendeleo vijijini na nyenzo muhimu katika kuboresha hali ya maisha ya watu, kuondoa umaskini na uhifadhi wa mazingira.

### Ngazi za Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi

Mipango ya matumizi bora ya ardhi huandaliwa na kutekelezwa katika ngazi mbalimbali ikiwemo:-

- Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi (National Land Use Framework Plan)
- Mipango ya Kanda ‘*Zonal/Regional Physical Plans*’
- Mpango wa Wilaya wa Matumizi ya Ardhi ‘*District Land Use Framework Plan*’
- Mpango wa Kijiji wa Matumizi Bora ya Ardhi.

### Mpango wa Kijiji wa Matumizi Bora ya Ardhi

Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kijiji ni utaratibu wa kutathmini na kupendekeza namna mbalimbali za matumizi ya maliasili/rasilimali ili kuinua hali ya maisha ya wanakijiji na kuondoa umaskini. Utaratibu wa kupanga, kutekeleza na kuhuisha matumizi ya ardhi unafaa zaidi iwapo utafanyika kwa njia ya ushirikishwaji, ikiwa na maana kuwa watumiaji wakubwa wa ardhi ambao ni wanakijiji wanashirikishwa kikamilifu. Ili kuhakikisha kuwa wanakijiji wanashiriki kikamilifu, ni muhimu kuzingatia makundi mbalimbali yaliyopo katika kijiji (k.v. wakulima, wafugaji, pamoja na jinsia na rika), ambayo yanaweza kuwa na utashi na malengo yanayotofautiana. Pia mipango hii ni njia muafaka ya kuainisha na kutenga ardhi ya mwekezaji kama vile, KILIMO KWANZA.

### Hatua za upangaji na utekelezaji

Mwongozo wa Ushirikishwaji Katika Mipango na Usimamizi wa Matumizi Bora ya Ardhi, unabainisha hatua kuu 6, katika mchakato wa upangaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi vijijini. Hatua hizi zinapitia mchakato mzima wa maandalizi wilayani, tathmini shirikishi kijijini, Ramani za matumizi ya ardhi, upangaji shirikishi, usalama wa miliki, hatua stahili za usimamizi wa ardhi.

Maandalizi Wilayani: Uhamasishaji, kuunda timu ya PLUM ya wilaya, na kuweka Mpango wa Utekelezaji wa PLUM wa wilaya.

- (ii) Tathmini shirikishi ya Matumizi ya Ardhi Vijijini (PRA): Uhamasishaji taasisi za kijiji; Elimu ya Sera na Sheria za Ardhi; Tathmini ya matumizi ya ardhi na raslimali; kubaini matatizo fursa na vikwazo; na kuweka Mpango Kazi wa Jamii- CAP).
- (iii) Matumizi ya Ardhi ya Kijiji: Kubaini, kuweka na kupima mipaka ya ardhi ya kijiji; utatuzi wa mogoro ya mipaka; Masjala ya Ardhi ya Wilaya; utoaji Cheti cha Ardhi ya Kijiji. Kuandaa ramani ya msingi ya matumizi ya ardhi ya kijiji (Existing land use map)
- (iv) Upangaji Matumizi Bora ya Ardhi ya Kijiji: Ushirikishwaji katika mipango na usimamizi; kuainisha hatua stahili za usimamizi (*appropriate land management measures*); na Sheria Ndogo za Usimamizi wa Matumizi Bora ya Ardhi. Kwa kufuata mpango kazi wa jamii, Halmashauri ya Kijiji kwa kutumia Kamati ya Usimamizi wa Ardhi ya Kijiji (VLUMC) huandaa rasimu ya mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji, ambayo baadaye huwasilishwa kwenye Mkutano wa Kijiji kujadiliwa ili kupelekea kwenye mpango kamili wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji.
- (v) Utawala wa Ardhi ya Kijiji: Masjala ya Ardhi ya Kijiji; Utoaji, usajili na usimamizi wa Hatimiliki za Kimila; na Utatuzi wa migogoro ya miliki.
- (vi) Hatua Stahili za Usimamizi: Upangaji na Utekelezaji wa Hatua Stahili za Usimamizi wa Ardhi na Uimarishaji mipango ya kina ya usimamizi wa matumizi ya ardhi kwa ushirikishaji na ujumuishaji sekta.

Kusoma kitabu chote, tembelea “*Reports and Publications*” inayopatikana kwenye tovuti hii.